

HALMASHAURI YA WILAYA YA WANGING'OMBE



12.02.2021

TANGAZO

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe anawatangazia wananchi wenye maeneo yaliyopimwa katika eneo la **Igwachanya** na **Chalowe** kuwa upimaji wake umekamilika.

Hivyo, wananchi wote mnatakiwa kufika ofisi za Ardhi Wilaya ukiwa na barua ya utambulisho kutoka Ofisi ya Serikali ya Kijiji husika, ukaguzi wa kiwanja utafanywa na wataalam ili kutambua kiwanja kinachoombewa kumilikishwa na ndipo utaruhusiwa kufanya malipo ya gharama za Upangaji, Upimaji na hatimaye gharama za umilikishaji.

Hatua za umilikaji wa kiwanja au viwanja zitafuata mara baada ya kukamilisha malipo ya upangaji, upimaji na umilikishaji kiwanja husika.

Aidha, gharama za awali kulipa ni zile zinazohusiana na kupanga na kupima, ambapo gharama za kuchangia zimeainishwa kwenye jedwali hapa chini kwa kila matumizi ya kiwanja husika. Na gharama za umilikishaji zitakokotolewa kulingana na ukubwa na matumizi ya kiwanja.

Fedha za Upangaji na upimaji zitalipwa kupitia Benki ya NMB - Akaunti ya Amana **60610003722** (Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe). Gharama na fedha za Umilikishaji zitalipwa benki au kwa njia ya simu baada ya kuandaliwa control namba.

Wananchi wote wenye viwanja mnatakiwa kufika ofisi za ardhi kwa ufafanuzi zaidi.

Tangazo limeandaliwa na

Edes P. Lukoa

Mkurugenzi Mtendaji (W)

Halmashauri ya Wilaya Wanging'ombe

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA WANGING'OMBE

Jedwali Na. 1: Mapendekezo ya Gharama za Viwanja kulingana na Matumizi

Na	Matumizi	Gharama kwa Kiwanja
1	Makazi	100,000
2	Makazi na Biashara	120,000
3	Biashara	150,000
4	Viwanda vidogo vidogo	200,000
5	Kituo cha Mafuta	500,000
6	Hoteli	250,000
7	Soko	100,000
8	Sehemu ya kuoeshea magari	100,000
9	Huduma za Kielimu	100,000
10	Huduma za Kiafya	100,000
11	Maegesho ya Magari	100,000
12	Majengo ya Umma	100,000
13	Viwanja vya Majengo ya Ibada	100,000
14	Housing Estate	100,000